VERMONT
DEPARTMENT OF HEALTH

Jifahamishe, Ukae Salama

Habari kutoka kwa Watoto wenye Mahitaji ya Afya ya Kipekee

Toleo la 4, Julai 2020

Mwanaharakati, mshairi, na mwandishi wa riwaya James Baldwin aliwahi kuandika *"Historia siyo yaliyopita, ni yanayoendelea sasa. Tunabeba historia yetu. Sisi ndio historia yetu."*

Tunapoendelea kushughulikia masuala changamano ya kimatibabu na kijamii yanayosababishwa na janga la COVID-19, tunatafuta nafasi za kusaidia familia zote za Vermont zenye mtoto au kijana aliye na mahitaji ya afya ya kipekee. Tunatumaini kwamba utaendelea kupata usaidizi kutoka kwa familia yako na jamii yako, na tunataka ujue kwamba hapa katika CSHN tumejitoea katika kujenga historia nzuri **pamoja**.

Masuala Muhimu:

***Taarifa za Mpango wa Tathmini ya Maendeleo ya CSHN/CDC*:**

Tunafurahia kutangaza kufunguliwa tena kwa Mpango wetu wa Tathmini ya Maendeleo ya CSHN ya Burlington mnamo Julai 1, 2020. Tutaanza kutoa tathmini za ana kwa ana katika barabara ya 1 South Prospect iliyoko Burlington, katika eneo la tathmini la Afya ya Watoto ya Ukuaji na Tabia (DB Peds) alipo Dkt. Beth Forbes. Tunapanga kurudisha shughuli katika 108 Cherry Street hivi karibuni, na kwa wakati huu tunaona hii ikiwa fursa nzuri ya ushirikiano wa ziada na washirika wetu wa UVMMC walioko katika DB Peds (Afya ya Watoto ya Ukuaji na Tabia) na katika Kliniki ya Kuchunguza Ugonjwa wa Akili wa Watoto iliyoko hali ambazo zimekuwa zikiongeza tathmni zao za ana kwa ana katika wiki za hivi karibuni.

Katika hali hii, tumekuwa wataalamu katika kuvaa vifaa vya pekee vya kujikinga (PPE). (Barakoa, vifaa vya kukinga uso, vifaa vya kukinga kupiga chafya, miwani, na vinginevyo!) Tumefaidika sana kutokana na kuratibu juhudi zetu na Afya ya Ndani ya UVMMC na VDH katika awamu zote za kupanga na kutayarisha huduma za kufungua tena. Bado hatuna tarehe maalum ya kufungua tena Kliniki ya Maendeleo ya Watoto (CDC) katika vituo vya Barre na Rutland, lakini tunatarajia kuwa na habari zaidi kuhusu jambo hilo katika wiki zijazo.

Asante kwa Timu yetu ya CDC kwa ubunifu, kutatua matatizo, ucheshi na usaidizi wa kila mtu katika nyakati hizi ngumu, na asanteni nyote kwa subira na kuelewa kwenu huku tukirudi katika kazi tunayofahamu na kupenda.

Kaa Salama,

Nora Sabo, MSW
Meneja wa Kliniki ya Maendeleo ya Watoto

VERMONT
DEPARTMENT OF HEALTH

Jifahamishe, Ukae Salama

Habari kutoka kwa Watoto wenye Mahitaji ya Afya ya Kipekee

Toleo la 4, Julai 2020

Nyenzo:

VT Medicaid: hutoa idhini ya huduma kwa ajili ya Chaguo la Utunzaji, Jeraha la Ubongo lenye Kufadhaisha, na Hali ya Dharura ya COVID -19 ya Utunzaji wa Kibinafsi wa Watoto hadi mwaka mmoja. Tathmini zitaruhusiwa kwa simu (soma mengi zaidi here).

Sauti za Familia: Taarifa yote kuhusu haki za kiraia, ubaguzi wa ulemavu, na utunzaji unaozingatia familia inaweza kupatikana kwenye Sauti za Familia website.

Kuzungumza na watoto kuhusu ukabila: Mwongozo kutoka kwa madaktari wa watoto na familia unaweza kupatikana here.

Habari ya Familia:

Hamjambo familia za CSHN, sisi ni familia ya Briggs. Will, Natalie na mimi (Amelia!) tunaishi mjini Shelburne na mbwa wetu wawili wanaoitwa Maverick na Cooper.

Natalie ana urudufishaji wa kromosomu; yeye ndiye mgonjwa pekee anayejulikana duniani aliye na urudufishaji huo. Maisha yetu katika miaka kumi iliyopita yamekuwa magumu kabisa, yenye kufadhaisha, kuvunja moyo, furaha, kusisimua, majivuno, kwa hivyo wakati ambapo janga lilitokea tulishikwa na hofu na kuogopa, lakini tuliamua haraka kwamba “tutashinda haya” na tukaanza kupanga. Hii ilimaanisha kuwa wabunifu, kufikiria zaidi ya yale tuliyofahamu. Tulikuwa tunajiuliza akilini tukiwa na msongamano wa mawazo, na woga **“Je, tutashughulikia vipi afya changamano ya kimatibabu ya mtoto wetu na kumlinda? Je, ni salama kwake kwenda hospitalini kwa ajili ya kudungwa dawa kila wiki na kuondolewa damu mara kwa mara? Je, ni salama kwa wauguzi wake wa utunzaji wa nyumbani kuja nyumbani kwetu? Je, ataendeleaje na elimu yake ya mbali kama mtoto Kiziwi/Kipofu? Je, nini kitatendeka endapo mmoja wetu atakuwa mgonjwa?”**

Nilishughulikia wasiwasi na woga wangu kwanza, niliacha kusoma makala ya habari, niliacha kusoma mambo mengi kwenye mitandao ya kijamii na kupunguza habari ambazo nilitazama. Niliwategemea timu ya kimatibabu ya Natalie ili itutolee taarifa sahihi na jinsi inavyotuathiri, hapa Vermont. Tuna bahati nzuri SANA kuwa na timu nzuri ya kimatibabu, kuanzia ofisi ya daktari wake wa watoto hadi timu ya UVMCH mpaka timu yake ya BCH, tumezungukwa na huduma nzuri, utunzaji na ujuzi.

VERMONT
DEPARTMENT OF HEALTH

Jifahamishe, Ukae Salama

Habari kutoka kwa Watoto wenye Mahitaji ya Afya ya Kipekee

Toleo la 4, Julai 2020

Tulijua, kama mambo yote ya kimatibabu, hatungejitegemea peke yetu. Tulihitaji msaada. Hatua yetu ya kwanza ilikuwa ni kuzungumza na daktari wetu wa watoto na kupitia orodha yetu ya wauguzi ili kuamua ikiwa wangeweza kushughulikia Natalie bila kumweka hatarini sana. Ilikuwa hivyo! Tungeweza kuendelea kupata utunzaji na usaidizi tuliouhitaji sana kutoka kwa wauguzi wetu. Katika masuala mengine. Iliamuliwa kwamba ilikuwa salama zaidi Natalie akibaki nyumbani kadri iwezekanavyo. Kupitia simu nyingi na madaktari, wauguzi, wafanyakazi walioko kazini mwa mume wangu na makampuni ya bima tuliweza kuhamisha kudungwa dawa kwa kila wiki kufanywe nyumbani, hata hivyo, huduma za udungwaji wa dawa wa nyumbani hazikuwa zinasajili mgonjwa yeyote mpya. Katika mpango wa ziada, tungeweza kujifunza jinsi ya kumpa sisi wenyewe. Kwa kila swali tulio kuwa nalo, tulipiga simu nyingi na kuwa na majadiliano ili kujua jinsi ya kuwa wabunifu, lakini kutopotoka ili bima iweze kuendelea kulipa. Tulihitaji kuwa wabunifu, lakini kama nyote mnavyojua, sisi ni wazazi wa mtoto mwenye mahitaji ya kipeee, tumefanya haya kwa miaka kumi.

AFYAMTANDAONI! Ni baraka na pia laana. Kama wengi wenu mnavyojua, kujaribu kumshughulikia mtoto na teknolojia inayohitajika ili kuwa na ziara ya mtandaoni ni kazi ngumu sana! Kwa bahati nzuri timu yetu iliyoko Boston ilitambua hili haraka sana na tuliweza kutuma picha na video kwenye barua pepe mapema ili zipitiwe kwa hivyo Natalie angekataa kushiriki, bado tungeweza kuwa na ziara yenye mafanikio na manufaa. Nyakati kama hizi ngumu, zinatuonyesha mambo mazuri yanayotokea katika jamii zetu, lakini pia zinatuonyesha mambo ambayo yanahitaji kushughulikiwa. Itabidi sisi wazazi/watunzaji tuseme mawazo na maoni yetu ili kutekeleza mabadiliko. Jimbo linapoendelea kufungua tena, wengi wetu tutaendelea kubaki nyumbani hadi chanjo na/au matibabu yapatikane. Je, baadhi ya mambo yanayoweza kukufaidi wewe na familia yako ni gani? Ikiwa yanakufaidi wewe, basi kuna uwezekano mkubwa kwamba yatafaidi watu wengine. Toa maoni yako kwa watoa huduma na marafiki zako, daima huwa kuna nafasi ya mabadiliko!

Tunawashukuru sana familia ya Briggs kwa kusimulia hadithi na mtazamo wao! Ikiwa ungependa kutuambia unachopitia katika kuwa na mtoto au kijana aliye na mahitaji ya afya ya kipekee, tafadhali wasiliana na Mratibu wa Ushirikiano wa Familia CSHN: charlotte.safran@partner.vermont.gov

Zungumza Nasi:

Wafanyakazi katika CSHN wamejitolea kukujulisha kuhusu nyenzo na sasisho za huduma ambazo zinaweza kufaa familia yako. Hata ingawa ziara za ana kwa ana zimesimamishwa kwa sasa, unaweza kutupigia simu au kututumia barua pepe. Nenda kwenye tovuti yetu ili upate CSHN Care Coordinator yako iliyoko karibuau tupigie simu katika 802-863-7338.

Pata taarifa na sasisho kwenye https://www.healthvermont.gov/family/special-health-needs .